JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# MWONGOZO WA UPIMAJI WA KITAIFA WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU DARASA LA II NGAZI YA SHULE

Kimetolewa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania
S. L. P. 2624
Dar es Salaam

**Julai, 2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# MWONGOZO WA UPIMAJI WA KITAIFA WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU DARASA LA II NGAZI YA SHULE

Kimetolewa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania
S. L. P. 2624
Dar es Salaam

**Julai, 2025**

## YALIYOMO

VIFUPISHO ........................................................................................iv
DIBAJI ........................................................................................ v
1.0 UTANGULIZI........................................................................ 1
2.0 UENDESHAJI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA: BASIC ENGLISH LANGUAGE SKILLS NA KUHESABU ........................................................................ 2
2.1 Usajili........................................................................................ 2
2.2 Maelekezo kuhusu Usajili wa Wanafunzi wa Upimaji .............. 3
2.2.1 Usajili katika Ngazi ya Shule .................................................. 3
2.2.2 Usajili katika Ngazi ya Kata na Wilaya .................................... 4
2.2.3 Usajili katika Ngazi ya Mkoa .................................................. 5
2.3 Upimaji wa Stadi za KKK na Miongozo ya Usahihishaji........... 5
2.4 Muundo wa Karatasi za Upimaji wa Stadi za KKK................. 13
2.4.1 Stadi ya Kusoma.......................................................... 13
2.4.2 Stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills.............. 14
2.4.3 Stadi ya Kuhesabu.......................................................... 16
2.5 Uandaaji na Upakiaji wa Zana za Upimaji wa KKK katika Mfumo wa PReM...................................................................... 18
2.6 Usimamizi wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu .............. 20
2.6.1 Upimaji wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu................... 20
2.6.2 Usimamizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ............... 22
2.7 Mafunzo ya Usimamizi wa Upimaji wa Stadi za KKK............ 22

2.8 Usimamizi na Ufuatiliaji wa Upimaji wa Stadi za KKK........... 23
2.8.1 Usimamizi wa Stadi za KKK................................................ 24
2.8.2 Ufuatiliaji wa Ufanyikaji wa Stadi za KKK.............................. 25
2.9 Usahihishaji wa Upimaji wa Stadi za KKK ............................. 25
2.9.1 Usimamizi wa Usahihishaji.................................................. 25
2.9.2 Utaratibu wa Usahihishaji wa Stadi ya Kusoma..................... 26
2.9.3 Utaratibu wa Usahihishaji wa Stadi za Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu.................................. 27
2.9.4 Uingizaji wa Alama na Uhakiki ............................................. 28
2.10 Uchakataji na Uchambuzi wa Matokeo ................................. 30
3.0 UANDAAJI WA TAARIFA KWA AJILI YA KUTOA MREJESHO ......................................................................... 32
4.0 HITIMISHO ......................................................................... 34

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| DEO | *District Education Officer* |
| EMIS | *Education Management Information System* |
| KKK | Stadi za Kusoma, Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu. |
| M2 | Fomu ya Mahudhurio ya Wanafunzi wa Darasa la II |
| PReM | *Primary Record Manager* |
| REO | *Regional Education Officer* |
| RITA | *Registration, Insolvency and Trusteeship Agency* |
| STNA | *Standard Two National Assessment* |
| WEO | *Ward Education Officer* |

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa mwongozo wa upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu (KKK) ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023 pamoja na Mitaala iliyoboreshwa ambapo msisitizo umewekwa katika kuboresha upimaji katika ngazi ya shule. Hivyo, Baraza limeandaa mwongozo ambao utatumika katika uendeshaji wa upimaji wa Stadi za KKK Kitaifa katika shule zote Tanzania Bara.

Mwongozo huu umetoa ufafanuzi wa kina kuhusu usajili wa wanafunzi wa Darasa la Pili. Pia unaonesha namna Upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu utakavyofanyika shuleni (School Based Assessment).

Mwongozo huu utatoa dira kwa wadau wote wa elimu watakaohusika kusimamia upimaji wa stadi za KKK Kitaifa ngazi ya shule kwa kubainisha michakato itakayofanyika kabla, wakati na baada ya usimamizi wa stadi hizo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliohusika katika kutayarisha mwongozo huu.

Prof. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Baraza la Mitihani la Tanzania lilianza kufanya upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) Darasa la II mwaka 2015. Upimaji huo ulifanyika kwa sampuli ukizingatia kanda za kielimu na ukijumuisha sampuli ya shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kufundishia. Kuanzia mwaka 2019 upimaji ulihusisha shule za serikali pekee zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia ambazo ziliteuliwa kwa kutumia njia ya sampuli nasibu kutoka katika kila halmashauri.

Kutokana na maboresho yaliyofanyika kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023 na Mitaala iliyoboreshwa, ilisisitizwa kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi. Hivyo, kuanzia mwaka 2025, upimaji utaanza kufanyika kwa wanafunzi wote Kitaifa ngazi ya shule. Upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu utawezesha kubainisha mafanikio pamoja na changamoto walizonazo wanafunzi wa Darasa la pili katika ujifunzaji wa Stadi za KKK. Taarifa itakayotokana na matokeo ya upimaji wa stadi hizo itawezesha walimu pamoja na mamlaka mbalimbali za elimu nchini kuchukua hatua za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi hizo. Mwongozo huu umeandaliwa ili kutoa dira ya namna upimaji huo utakavyoendeshwa.

Aidha, mwongozo umelenga kuwasaidia walimu wanaofundisha ngazi ya Darasa la Pili kubainisha maudhui yatakayopimwa na kuwawezesha kuelewa mambo mbalimbali yatakayozingatiwa wakati wa upimaji. Pamoja na mambo mengine, mwongozo umetoa maelekezo ya namna upimaji utakavyosimamiwa wakati unafanyika, usahihishaji, uingizaji wa alama kwenye mfumo wa PReM na uandaaji wa ripoti pamoja na namna ripoti hizo zitakavyosambazwa na kuwafikia walengwa.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa, wadau wote wa elimu watasoma na kuuelewa mwongozo huu na kuutumia ipasavyo wakati wa upimaji ili kuongeza ubora wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Msingi.

## 2.0 UENDESHAJI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA: BASIC ENGLISH LANGUAGE SKILLS NA KUHESABU

### 2.1 Usajili

Usajili wa wanafunzi utafanywa na Mkuu wa Shule kwa kushirikiana na Mwalimu wa Taaluma pamoja na Mwalimu wa Darasa kwa kutumia mfumo wa PReM kwa kalenda itakayotolewa na Baraza la Mitihani.

Kazi ya kusasisha taarifa za wanafunzi wa Darasa la Pili itafanyika ndani ya kipindi cha usajili.

## 2.2 Maelekezo kuhusu Usajili wa Wanafunzi wa Upimaji

Maelekezo muhimu yanayohusu usajili wa wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili (STNA) ni yafuatayo:

### 2.2.1 Usajili katika Ngazi ya Shule

Usajili katika ngazi ya Shule utafanywa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

**(a) Uhakiki wa Fomu za Mahudhurio ya Usajili (M2)**

Mkuu wa Shule akishirikiana na Mwalimu wa Taaluma pamoja na Mwalimu wa Darasa husika afanye uhakiki wa usahihi wa taarifa zilizopo katika Fomu ya Mahudhurio ya Usajili Darasa la Pili (M2). Zoezi hili lifanywe kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha kuwa taarifa za usajili kwenye Fomu za M2 zinafanana na taarifa zilizopo kwenye mfumo wa kutunza Taarifa za usajili wa wanafunzi Elimu ya Msingi (PReM).

**(b) Uthibitisho wa Kukamilika kwa Usajili**

(i) Mkuu wa Shule akikamilisha vipengele vyote kuhusu kuhakiki taarifa za usajili

wa wanafunzi wa STNA atathibitisha usajili kwenye mfumo. Usajili ukishathibitishwa Mkuu wa Shule hataweza kuhariri tena.

(ii) Mkuu wa Shule atachapa nakala **mbili (2)** za M2 kisha wanafunzi wataweka saini zao katika fomu hizo. Mwanafunzi anatakiwa kusaini kwa kuandika jina lake la kwanza na la pili kwa kifupi (initials) na jina la ukoo kwa ukamilifu (Mfano; M. J. Ndosa). Wanafunzi wasiweke saini za kukoroga. Aidha, Mkuu wa Shule atasaini na kisha kugonga muhuri katika Fomu hizo.

(iii) Mkuu wa Shule atawasilisha nakala za Fomu ya M2 kwa Afisa Elimu wa Wilaya (DEO) kwa ajili ya uthibitisho kuwa usajili umekamilika.

### 2.2.2 Usajili katika Ngazi ya Kata na Wilaya

Katika ngazi ya Kata na Wilaya, Afisa Elimu Kata (WEO) na Afisa Elimu wa Wilaya (DEO) kwa kushirikiana na Wakuu wa Shule wataendesha zoezi la uhakiki wa usajili wa wanafunzi ili kuona kama taarifa za wanafunzi

kwenye PReM zinaoana na taarifa za M2. Aidha, watahakiki kuona kama wanafunzi wote wamejaziwa taarifa zote kwa mujibu wa matakwa ya PReM.

#### 2.2.3 Usajili katika Ngazi ya Mkoa

(a) Afisa Elimu wa Mkoa (REO) atapokea taarifa za usajili wa wanafunzi wa STNA za Halmashauri zote zilizopo katika Mkoa wake.

(b) REO ataandaa taarifa kuhusu kukamilika kwa zoezi la usajili wa STNA na kutuma au kuwasilisha kwa Katibu Mtendaji.

#### 2.2.4 Usajili wa Wanafunzi wanaotoka Nje ya Nchi

Wanafunzi wa Darasa la Pili wanaotoka nje ya nchi watasajiliwa baada ya kupata kibali kutoka kwa Kamishna wa Elimu na kuwasilisha maombi Baraza la Mitihani kwa ajili ya kupewa namba ya PReM.

### 2.3 Upimaji wa Stadi za KKK na Miongozo ya Usahihishaji

Maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Pili katika Stadi za Kusoma, Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu yataandaliwa kwa kuzingatia Sera ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023, Mtaala

ulioboreshwa na Muhtasari wa kufundishia Darasa la Kwanza na la Pili. Stadi mbalimbali zitapimwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la 1 – 3.

Jedwali la utahini litaandaliwa na kutumika katika kuandaa maswali ili kuwa na msambao wa maswali unaopima umahiri katika ngazi zote sita za utambuzi za Benjamin Bloom (Bloom Taxanomy).

**Jedwali la 1: Stadi ya Kusoma**

| NA. | STADI KUU | STADI MAHUSUSI | UPIMAJI | UPIMAJI WA VIWANGO VYA UTENDAJI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji Hafifu** | **Utendaji wa Wastani** | **Utendaji Mzuri** | **Utendaji Mzuri Sana** |
| 1. | Kusoma | Kusoma kwa ufasaha | Uwezo wa mwanafunzi katika kusoma maneno 50 kwa dakika moja katika kifungu cha habari kwa sauti na kwa kasi stahiki. | Kusoma kwa usahihi maneno **0-12** | Kusoma kwa usahihi maneno **13-25** | Kusoma kwa usahihi maneno **26-35** | Kusoma kwa usahihi maneno **36-50** |
| | | Kusoma na kusikiliza kwa ufahamu | Uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali 5 atakayoulizwa kwa mdomo. | Kujibu maswali **0-1** | Kujibu maswali **2-3** | Kujibu maswali **4** | Kujibu maswali yote **5** |

**Jedwali la 2: Stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills**

| NA. | STADI KUU | STADI MAHUSUSI | UPIMAJI | UPIMAJI WA VIWANGO VYA UTENDAJI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji Hafifu** | **Utendaji wa Wastani** | **Utendaji Mzuri** | **Utendaji Mzuri Sana** |
| 1. | Kuandika | Kutofautisha herufi kubwa na ndogo katika maneno | Uwezo wa mwanafunzi katika kuandika maneno 5 kwa usahihi atakayopewa. | Kuandika kwa usahihi maneno **0 - 1** | Kuandika kwa usahihi maneno **2 - 3** | Kuandika kwa usahihi maneno **4** | Kuandika kwa usahihi maneno **5** |
| | | Kuandika maneno kwa kutumia picha za vitu mbalimbali | Uwezo wa mwanafunzi wa kuandika majina ya picha za vitu **5** kuhusu majina ya matunda, wanyama, vifaa vya ndani nk. | Kuandika kwa usahihi majina **0 - 1** | Kuandika kwa usahihi majina **2 - 3** | Kuandika kwa usahihi majina **4** | Kuandika kwa usahihi majina **5** |
| | | Kutumia kanuni za uandishi | Uwezo wa kunakili hadithi fupi/kifungu cha maneno na kuweka alama nne za uandishi kwa usahihi. | Kunakili kwa usahihi maneno 0-4 na kutumia alama **1** | Kunakili kwa usahihi maneno 5-8 na kutumia alama **2** | Kunakili kwa usahihi maneno 9-12 na kutumia alama **3** | Kunakili kwa usahihi maneno 13-16 na kutumia alama za uandishi zote **4** |
| | | Kuandika matini kwa kufuata mtiririko wenye mantiki | Uwezo wa kuandika na kupanga sentensi kwa kufuata mtiririko wenye mantiki. | Kuandika na kupanga kwa usahihi sentensi **0 - 1** | Kuandika na kupanga kwa usahihi sentensi **2 - 3** | Kuandika na kupanga kwa usahihi sentensi **4** | Kuandika na kupanga kwa usahihi sentensi **5** |

| NA. | STADI KUU | STADI MAHUSUSI | UPIMAJI | UPIMAJI WA VIWANGO VYA UTENDAJI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji Hafifu** | **Utendaji wa Wastani** | **Utendaji Mzuri** | **Utendaji Mzuri Sana** |
| 2. | *Demonstrate Mastery of Basic English Language Skills* | *Develop early literacy and numeracy skills* | Uwezo wa mwanafunzi wa kuandika maneno atakayosomewa na msimamizi kama vile; *bag*, *ten*, *did*, *dog* na *sun*. | Kuandika kwa usahihi maneno **0 - 1** | Kuandika kwa usahihi maneno **2 - 3** | Kuandika kwa usahihi maneno **4** | Kuandika kwa usahihi maneno **5** |

**Jedwali la 3: Stadi ya Kuhesabu**

| NA | STADI KUU | STADI MAHUSUSI | UPIMAJI | UPIMAJI WA VIWANGO VYA UTENDAJI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **Utendaji Hafifu** | **Utendaji wa Wastani** | **Utendaji Mzuri** | **Utendaji Mzuri Sana** |
| 1 | Kuhesabu | Kutambua Dhana ya Namba | Uwezo wa kubaini namba kuanzia 1 – 100 kwa tarakimu na kwa maneno katika swali lenye vipengele vitano. | Kubaini namba kuanzia 1 – 100 kwa tarakimu na kwa maneno kwa usahihi katika kipengele kimoja au viwili kati ya vitano. | Kubaini namba kuanzia 1 – 100 kwa tarakimu na kwa maneno katika vipengele vitatu kati ya vitano kwa usahihi. | Kubaini namba kuanzia 1 – 100 kwa tarakimu na kwa maneno katika vipengele vinne kati ya vitano kwa usahihi. | Kubaini namba kuanzia 1 – 100 kwa tarakimu na kwa maneno katika vipengele vyote vitano kwa usahihi. |
| | | | Uwezo wa kupanga namba kwa mfuatano katika swali moja lenye vipengele vitano. | Kupanga namba kwa mfuatano kwa usahihi katika kipengele kimoja au viwili kati ya vitano. | Kupanga namba kwa mfuatano kwa usahihi katika vipengele vitatu kati ya vitano. | Kupanga namba kwa mfuatano kwa usahihi katika vipengele vinne kati ya vitano. | Kupanga namba kwa mfuatano kwa usahihi katika vipengele vyote vitano. |
| | | Kutumia Matendo ya Kihisabati | Uwezo wa kujumlisha na kupata jumla isiyozidi 999 katika maswali matano. | Kujumlisha na kupata jumla isiyozidi 999 katika swali moja kwa usahihi. | Kujumlisha na kupata jumla isiyozidi 999 katika maswali mawili kwa usahihi. | Kujumlisha na kupata jumla isiyozidi 999 katika maswali manne kati ya maswali matano kwa usahihi. | Kujumlisha na kupata jumla isiyozidi 999 katika maswali yote matano kwa usahihi. |

| NA | STADI KUU | STADI MAHUSUSI | UPIMAJI | UPIMAJI WA VIWANGO VYA UTENDAJI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Hafifu | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana |
| | | | Uwezo wa kutoa namba zisizozidi 999 katika maswali matano. | Kutoa namba zisizozidi 999 katika kipengele kimoja au viwili kati ya vitano. | Kutoa namba zisizozidi 999 katika vipengele vitatu kati ya vitano. | Kutoa namba zisizozidi 999 katika maswali manne kati ya maswali matano kwa usahihi. | Kutoa namba zisizozidi 999 katika maswali yote matano kwa usahihi. |
| | | | Uwezo wa kuzidisha namba kwa namba yenye tarakimu moja na kupata zao lisilozidi 100 katika maswali matano. | Kuzidisha namba kwa namba yenye tarakimu moja kwa usahihi na kupata zao lisilozidi 100 katika kipengele kimoja au viwili kati ya vitano. | Kuzidisha namba kwa namba yenye tarakimu moja na kupata zao lisilozidi 100 katika vipengele vitatu kati ya vitano. | Kuzidisha namba kwa namba yenye tarakimu moja na kupata zao lisilozidi 100 katika maswali manne kwa usahihi. | Kuzidisha namba kwa namba yenye tarakimu moja na kupata zao lisilozidi 100 katika maswali yote matano kwa usahihi. |
| | | | Uwezo wa kugawanya namba zisizozidi 100 bila baki katika maswali matano. | Kugawanya namba zisizozidi 100 bila baki katika kipengele kimoja au viwili kati ya vitano. | Kugawanya namba zisizozidi 100 bila baki katika vipengele vitatu kwa usahihi. | Kugawanya namba zisizozidi 100 bila baki katika maswali manne kwa usahihi. | Kugawanya namba zisizozidi 100 bila baki katika maswali yote matano kwa usahihi. |

| NA | STADI KUU | STADI MAHUSUSI | UPIMAJI | UPIMAJI WA VIWANGO VYA UTENDAJI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Utendaji Hafifu | Utendaji wa Wastani | Utendaji Mzuri | Utendaji Mzuri Sana |
| | | Kutumia Dhana za Kihisabati | Uwezo wa kubaini maumbo ya msingi matano. | Kubaini umbo moja au mawili kati ya maumbo matano kwa usahihi. | Kubaini maumbo matatu kati ya maumbo matano kwa usahihi. | Kubaini maumbo manne kati ya maumbo matano kwa usahihi. | Kubaini maumbo yote matano kwa usahihi. |
| | | | Uwezo wa kutambua robo, theluthi, nusu na theluthi mbili ya kitu kizima ili kujenga dhana ya utambuzi wa sehemu katika vitu vizima vitano. | Kutambua sehemu moja au mbili kati ya sehemu tano kwa usahihi. | Kutambua sehemu tatu kati ya tano kwa usahihi. | Kutambua sehemu tatu kati ya tano kwa usahihi. | Kutambua sehemu zote tano kwa usahihi. |

## 2.4 Muundo wa Karatasi za Upimaji wa Stadi za KKK

### 2.4.1 Stadi ya Kusoma

(a) Upimaji wa stadi ya Kusoma utakuwa na maswali **mawili (2)**. Swali la kwanza litapima uwezo wa wanafunzi kusoma kifungu chenye **maneno 50** kwa **dakika moja** na **kwa ufasaha**. Kila neno katika kifungu hicho kitakuwa na alama **00½** hivyo, swali hili litakuwa na alama **25**. Katika swali la pili, wanafunzi watasoma kifungu hicho hicho kwa mara ya pili na kuulizwa maswali katika kipengele (a) – (e) ili kuwapima stadi za ufahamu. Swali hili litakuwa na alama **25** sawa na alama **5** kwa kila kipengele.

(b) Upimaji wa stadi ya Kusoma utafanyika kwa muda wa **dakika kumi (10)** kwa kila mwanafunzi na dakika **kumi na tano (15)** kwa wanafunzi **wenye mahitaji maalumu**.

(c) Alama za upimaji wa Kusoma kwa kila mwanafunzi zitarekodiwa kwenye **nakala ngumu ya fomu ya Kiolezo**

iliyopakuliwa kutoka katika mfumo wa PReM atakayopewa msimamizi.

### 2.4.2 Stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills

(a) Upimaji wa Stadi ya Kuandika: Basic Language Skills utafanyika kwa dakika **arobaini (40)** na dakika **hamsini (50)** kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Karatasi ya Stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills itajumuisha swali moja kutoka katika Umahiri Mkuu wa *Demonstrate Mastery of Basic English Language Skills*. Swali hilo litafanyika kwa kutumia lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wote.

(b) Karatasi ya upimaji wa Stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills itakuwa na maswali **manne (4)** kutoka katika umahiri mahsusi wa aina nne.

(i) Swali la kwanza litapima uwezo wa mwanafunzi wa kusikiliza na kuandika maneno ya kawaida

**kumi (10)** ya lugha ya Kiingereza kutoka katika Umahiri Mahususi wa *Develop Early Literacy and Numeracy Skills*. Kila neno litakuwa na alama **00½** hivyo, swali hili litakuwa na alama **tano (05)**.

(ii) Swali la pili litapima uwezo wa wanafunzi wa kuandika majina ya picha **tano (5)** kwa usahihi au uwezo wa mwanafunzi wa kuandika herufi kubwa au ndogo katika maneno **matano (5)**. Kila kipengele kitakuwa na alama **moja (01)** hivyo, swali hili litakuwa na alama **tano (05)**.

(iii) Swali la tatu litapima uwezo wa wanafunzi wa kunakili maneno **kumi na sita (16)** na kutumia alama **nne (4)** za uandishi katika sentensi ambazo ni: nukta (.), mkato (,), mshangao (!) na kiulizo (?). Kila neno na kila alama ya uandishi itakuwa na alama **moja (01)** hivyo, swali hili litakuwa na alama **ishirini (20)**.

(iv) Swali la nne litapima uwezo wa wanafunzi kuandika matini fupi kwa mtiririko wa matukio wenye mantiki. Mwanafunzi atapanga na kuandika upya katika mpangilio unaoleta mantiki sentensi **tano (5)** zilizochanganywa. Kila sentensi itakuwa na jumla ya maneno **manne (04)** na kila neno kwenye sentensi iliyopangwa kwa usahihi litakuwa na alama **moja (01)**. Hivyo, swali hili litakuwa na alama **ishirini (20)**.

### 2.4.3 Stadi ya Kuhesabu

(a) Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu utafanyika kwa muda wa **dakika hamsini (50)** kwa wanafunzi wa kawaida, na wanafunzi **wenye mahitaji maalumu** watafanya kwa muda wa **saa moja (1)**.

(b) Karatasi ya Stadi ya Kuhesabu itakuwa na maswali **ishirini** (**20**) ambayo wanafunzi watatakiwa kukokotoa kwa kutumia matendo ya namba ya kihisabati ya **kujumlisha**, **kutoa**, **kuzidisha** na **kugawanya**.

Maswali hayo yatakuwa kama ifuatavyo:

(i) Swali la **1 – 5** yatapima umahiri wa wanafunzi katika dhana ya namba kuhusu mfululizo na kubaini namba kuanzia 1 – 100 kwa tarakimu na kwa maneno. Kila swali katika kundi hili litakuwa na alama **mbili (02)** hivyo, kuwa na jumla ya alama **kumi (10)**.

(ii) Swali la **6 – 10** yatapima uwezo wa wanafunzi kutumia matendo ya kihisabati. Wanafunzi watatakiwa kujumlisha au kutoa namba zisizozidi 999. Swali la 6 – 8 yatakuwa na alama **mbili (02)** kila swali, wakati swali la 9 na 10 kila swali litakuwa na alama **tatu (03)**. Hivyo, kuwa na jumla ya alama **kumi na mbili (12)**.

(iii) Swali la **11 – 15** yatapima uwezo wa wanafunzi kuzidisha namba kwa namba yenye tarakimu moja

na kupata zao lisilozidi 100. Pia, wanafunzi watatakiwa kugawanya namba zisizozidi 100 bila baki. Kila swali katika kundi hili litakuwa na alama **tatu (03)** na kufanya jumla ya alama **kumi na tano (15)**.

(iv) Swali la **16 – 20** yatapima uwezo wa wanafunzi kutumia dhana za kihisabati. Wanafunzi watatakiwa kubaini maumbo ya msingi. Aidha, wanafunzi watatakiwa kutumia vitu vizima kutambua robo, theluthi, nusu na theluthi mbili ya kitu kizima. Swali la 16 na 17 yatakuwa na alama **mbili (02)** kila swali, wakati swali la 18 hadi 20 kila swali litakuwa na alama **tatu (03)** na kufanya jumla ya alama **kumi na tatu (13)**.

## 2.5 Uandaaji na Upakiaji wa Zana za Upimaji wa KKK katika Mfumo wa PReM

Uandaaji wa zana za upimaji wa stadi za KKK utafanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Zana hizo zitapatikana katika mfumo wa PReM ambapo Mkuu wa Shule atatakiwa kuzipakua. Hivyo, uandaaji wa zana hizo kwa ajili ya ufanyikaji wa Upimaji utafanywa katika ngazi ya shule kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:

(a) Baraza la Mitihani la Tanzania litaweka nakala laini (Portable Document Format) za zana za Upimaji wa Stadi za KKK katika mfumo wa PReM.

(b) Mkuu wa Shule atawezeshwa kupakua (Download) zana za upimaji wa stadi za KKK kupitia dirisha lililowekwa kwenye mfumo kwa ajili ya kufanya maandalizi ya Upimaji wa zana husika.

(c) Zana za Stadi ya Kusoma, ziandaliwe kulingana na idadi ya mikondo ya kusoma katika shule husika. Aidha, fomu za kiolezo zipakuliwe kulingana na idadi ya mikondo ambapo mkondo **mmoja (1)** utakuwa na wanafunzi **ishirini (20)**.

(d) Zana za Stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu, ziandaliwe kulingana na idadi ya wanafunzi.

(e) Zana za wanafunzi wenye Mahitaji Maalum ziandaliwe kulingana na mahitaji ya wanafunzi husika.

(f) Karatasi zote zilizoandaliwa ziwekwe katika bahasha za khaki (A3) na kuhifadhiwa katika Kasiki kabla ya kupelekwa kwenye chumba cha Upimaji. Zana zote za upimaji ziwe zimekamilika kupakuliwa (Downloaded) siku tano (5) kabla ya ufanyikaji wa upimaji.

## 2.6 Usimamizi wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

### 2.6.1 Upimaji wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Upimaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu utazingatia makundi ya wanafunzi wenye ulemavu wa uoni, uziwi na ulemavu wa viungo. Makundi hayo yatapimwa baada ya kubainisha mahitaji yao kwenye usajili. Upimaji utafanyika kama ifuatavyo;

(a) Wanafunzi wenye Uoni Hafifu (Low Vision).

Wanafunzi wenye uoni hafifu watafanya upimaji unaofanywa na

wanafunzi wa kawaida isipokuwa, upimaji utaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji yao.

(b) Wanafunzi Wasioona

(i) Upimaji wa stadi zote utaandaliwa kulingana na mahitaji ya wanafunzi husika.

(ii) Maswali yanayohusu picha, ramani na michoro yatabadilishwa na kuwa katika maelezo.

(c) Wanafunzi wenye Uziwi

(i) Upimaji wa stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu utaandaliwa sawa na wanafunzi wengine. Aidha, katika stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills endapo kutakuwa na swali la imla, wanafunzi hao watapewa swali mbadala.

(ii) Katika stadi ya Kusoma, mwanafunzi atapewa karatasi yenye kifungu cha maneno na kukisoma kisha kujibu maswali

yanayohusu kifungu hicho kwa kuandika.

(d) Wanafunzi wenye Ulemavu wa Viungo

Mwanafunzi mwenye mahitaji ya kiupimaji ambaye ana ulemavu zaidi ya mmoja unaomfanya kushindwa kusoma na kuandika atapimwa kwa kuzingatia mahitaji maalum ya **uhitaji alionao**.

### 2.6.2 Usimamizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu

Wanafunzi watasimamiwa na wasimamizi wenye utaalamu wa fani husika kwa kuzingatia aina ya ulemavu walionao.

## 2.7 Mafunzo ya Usimamizi wa Upimaji wa Stadi za KKK

Mafunzo ya usimamizi wa upimaji wa stadi za KKK yatafanyika kwa makundi matatu kama ifuatavyo:

(a) Kundi la kwanza litahusisha Maafisa Mitihani, Maafisa Usajili na Maafisa TEHAMA wa Baraza la Mitihani ambao watateuliwa kufanya kazi hiyo. Sekretarieti ya

Uendeshaji wa KKK itatoa mafunzo kwa kundi hili.

(b) Kundi la pili litahusisha Maafisa Elimu Mkoa na Maafisa Elimu wa Wilaya pamoja na Maafisa Elimu Taaluma Mkoa na Wilaya, Mthibiti Ubora wa Shule kwa kila Halmashauri pamoja na Waratibu Elimu Kata wote katika Halmashauri. Wawezeshaji wa kundi hili watakuwa ni Maafisa Mitihani, Maafisa Usajili na Maafisa TEHAMA waliopewa mafunzo na Sekretarieti ya KKK.

(c) Kundi la tatu litahusisha Walimu Wakuu pamoja na Walimu watakaoteuliwa kushiriki usimamizi ambao watapewa mafunzo yatakayotolewa na Waratibu Elimu Kata.

## 2.8 Usimamizi na Ufuatiliaji wa Upimaji wa Stadi za KKK

Usimamizi wa stadi za KKK utafanywa na walimu watakaoteuliwa na Mkuu wa Shule kulingana na idadi ya wanafunzi katika shule husika au itakavyoamriwa na mamlaka husika. Aidha, ufuatiliaji wa Upimaji wa stadi za KKK utafanywa na Baraza la Mitihani kwa kushirikiana na wadau wengine.

### 2.8.1 Usimamizi wa Stadi za KKK

(a) Katika upimaji wa stadi za Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu, wanafunzi watafanya upimaji kama wanavyofanya upimaji wa kawaida unaoendeshwa shuleni. Aidha, stadi ya Kusoma itahusisha usomaji wa mwanafunzi mmoja mmoja, hivyo Mkuu wa Shule atapanga wasimamizi katika namna bora ambayo kila mwanafunzi atapata fursa ya kusoma kulingana na mwongozo wa stadi ya Kusoma.

(b) Mkuu wa Shule atachapa nakala **moja (1)** ya M2 kisha Msimamizi atahakiki mahudhurio ya kila mwanafunzi kwa kuweka alama ya vema **(✓)** kwa mwanafunzi atakayefanya Upimaji na alama ya kosa **(x)** kwa ambaye hatafanya. Aidha, Mkuu wa Shule atasaini na kisha kugonga muhuri katika Fomu hiyo.

(c) Mkuu wa Shule atazihifadhi nakala za Fomu ya M2 pamoja na karatasi za Upimaji zilizosahihishwa kwa rejea.

### 2.8.2 Ufuatiliaji wa Ufanyikaji wa Stadi za KKK

Baraza la Mitihani kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni TAMISEMI, WyEST, ofisi ya Elimu Mkoa na Wilaya, Wathibiti Ubora kwa kila Halmashauri pamoja na Maafisa Elimu Kata watafanya ufuatiliaji wa kina ili kuhakikisha Upimaji unafanyika kwa kufuata miongozo iliyoandaliwa.

## 2.9 Usahihishaji wa Upimaji wa Stadi za KKK

Usahihishaji wa karatasi za upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu utafanyika shuleni kwa mujibu wa miongozo itakayotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Miongozo hiyo utapandishwa katika mfumo wa PReM ambapo kila Mkuu wa Shule atatakiwa kupakua na kuwapa walimu husika kutumia wakati wa usahihishaji.

### 2.9.1 Usimamizi wa Usahihishaji

(a) Usahihishaji wa karatasi za upimaji wa stadi ya Kusoma, Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu utafanywa na walimu watakaoteuliwa na Mkuu wa Shule husika.

(b) Mkuu wa Shule atahakikisha kuwa kazi ya usahihishaji inafanyika shuleni katika mazingira tulivu kwa kuzingatia ratiba ya kazi na utaratibu wa usahihishaji kwa kila stadi.

(c) Baraza la Mitihani likishirikiana na Afisa Elimu Mkoa, Wilaya na Kata itafanya ufuatiliaji wa usahihishaji wa upimaji wa stadi za KKK ili kuhakikisha kuwa kazi hiyo inafanywa kwa kufuata utaratibu na mwongozo uliowekwa.

### 2.9.2 Utaratibu wa Usahihishaji wa Stadi ya Kusoma

(a) Usahihishaji wa karatasi ya Upimaji wa stadi ya Kusoma utafanywa na msimamizi wakati mwanafunzi atakapokuwa anasoma.

(b) Msimamizi atatakiwa kutumia *stop watch* ili kuweza kurekodi muda aliotumia mwanafunzi katika kusoma kifungu cha habari kwa ufasaha.

(c) Alama za stadi ya Kusoma zitarekodiwa na msimamizi moja kwa moja wakati wa upimaji kwa kujaza katika nakala ngumu ya fomu ya

kiolezo wakati mwanafunzi atakapokuwa anasoma.

(d) Mkuu wa Shule atatakiwa kuteua walimu watakaofanya uhakiki wa uingizaji wa alama kwa kuhakiki alama zilizoingizwa kwenye kiolezo (template) cha nakala ngumu na laini.

### 2.9.3 Utaratibu wa Usahihishaji wa Stadi za Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu

(a) Wasahihishaji watatumia kalamu ya wino mwekundu kuweka alama ya vema ☑ kwenye jibu lililo sahihi na alama ya kosa ☒ kwenye jibu lisilo sahihi.

(b) Baada ya usahihishaji wa skripti, uhakiki wa usahihishaji utafanyika kwa makini ili kuona kuwa kila swali limesahihishwa na alama zimeandikwa kwa usahihi. Aidha, uhakiki utafanyika ili kuona kama ujumlishaji umefanyika vema kwenye skripti ya kila mwanafunzi.

### 2.9.4 Uingizaji wa Alama na Uhakiki

Mfumo wa PReM utatumika katika kunasa alama ghafi zote. Mwalimu atabainisha wanafunzi wote ambao hawakufanya upimaji katika ngazi ya kila stadi kupitia mfumo huu.

Alama za wanafunzi katika stadi zote zitaingizwa kwenye kiolezo (template) ambacho kitakuwa na muonekano maalumu unaofaa kwa ajili ya kuingizia alama za stadi husika. Violezo vyote vitakuwa na namba na jina la mwanafunzi, mahudhurio na visanduku kwa ajili ya kujaza alama.

Taarifa za namba na majina ya wanafunzi yatatoka moja kwa moja kutoka kwenye mfumo na mwalimu hataweza kubadilisha taarifa hizo.

Mwalimu akipakua kiolezo atatakiwa kuingiza alama kwenye fomu ya kiolezo ambapo ataandika sifuri (0) kwenye visanduku vya maswali ambavyo mwanafunzi amekosa.

Kwa maswali ambayo mwanafunzi atakuwa amepata, visanduku vyake vitaachwa wazi. Wakati wa kupandisha kiolezo, mfumo utakagua alama za kila mwanafunzi kwa stadi husika na utatoa ripoti fupi inayobainisha idadi ya wanafunzi waliopandishiwa alama zao kwa usahihi na wanafunzi ambao alama zao hazikupanda kwenye mfumo kutokana na kutofautiana kwa taarifa, kwa mfano mwanafunzi mtoro kuwa na alama.

Mfumo wa PReM utamwezesha mwalimu kupakua ripoti ya jumla ya uingizaji wa alama ambayo itaonesha orodha ya wanafunzi na mahudhurio yao kwenye kila stadi.

Kupitia ripoti hii, mwalimu ataweza kubaini changamoto za uingizaji wa alama na ataweza kufanya maboresho maeneo yote yenye dosari. Pia, mwalimu atawezeshwa kupakua ripoti za List 1 na List 2 kwa uhakiki. Ripoti hizo kwa stadi husika zitatoka ikiwa uingizwaji wa alama zake umekamilika.

## 2.10 Uchakataji na Uchambuzi wa Matokeo

Uchambuzi wa matokeo na utoaji wa matokeo ya wanafunzi waliofanya upimaji wa KKK utafanywa kama ifuatavyo:

(a) Taarifa za Usajili zitapandishwa kwenye Kanzidata ya EMIS kwa ajili ya uchakataji na utoaji wa matokeo ya jumla (Mfumo kwa Mfumo).

(b) Alama za jumla za mwanafunzi na za kila swali katika stadi zote zitapakuliwa kutoka kwenye mfumo wa PReM kwa ajili ya uchambuzi.

(c) Fomu ya mahudhurio itapakuliwa kwenye mfumo kwa ajili ya kuhifadhi rekodi za waliofanya na wasiofanya Upimaji kwa ajili ya uhakiki wa taarifa wakati wa uchakataji wa matokeo.

(d) Uchambuzi wa matokeo ya wanafunzi utafanyika ili kubaini yafuatayo katika kila stadi:
   (i) Katika Stadi ya Kusoma wanafunzi wanaoweza na wasioweza kusoma na kusikiliza kwa ufahamu.

(ii) Katika Stadi ya Kuandika: Basic English Language Skills

- Wanaoweza na wasioweza kuandika maneno ya Kiingereza wanayosomewa.

- Wanaoweza na wasioweza kutofautisha herufi kubwa na ndogo.

- Wanaoweza na wasioweza kunakili kifungu cha habari na kutumia kanuni za uandishi.

- Wanaoweza na wasioweza kuandika matini kwa kufuata mtiririko wenye mantiki.

- Wanaoweza na wasioweza kuandika maneno kwa kutumia picha za vitu mbalimbali.

(iii) Katika Stadi ya Kuhesabu:

- Wanaoweza na wasioweza kutambua dhana ya namba.

- Wanaoweza na wasioweza kutumia matendo ya kihisabati.

- Wanaoweza na wasioweza kutumia dhana za kihisabati.

## 3.0 UANDAAJI WA TAARIFA KWA AJILI YA KUTOA MREJESHO

Taarifa za upimaji wa Stadi za KKK zitaandaliwa kulingana na vigezo vilivyowekwa kwenye mwongozo wa upimaji ambavyo vinatokana na maudhui yanayofundishwa Darasa la I na la II. Maudhui hayo yanayotokana na mtaala wa Elimu ya Msingi katika ngazi husika sambamba na mihtasari ya Stadi za KKK iliyotumika katika kuandaa zana za upimaji. Vigezo hivyo ni pamoja na utendaji hafifu, utendaji wa wastani utendaji mzuri na utendaji mzuri sana.

Takwimu zitawasilishwa kwa kutumia takwimu elezi (descriptive statistics) zikihusisha takwimu tarakimu (quantitavie data) na takwimu kimaelezo (qualitative data). Majedwali na vielelezo mbalimbali vitatumika kuwasilisha taarifa hizo. Uwasilishaji utafanyika ili kuhakikisha kuwa walengwa kama vile walimu, maafisa elimu wa ngazi mbalimbali, wathibiti ubora na wadau wengine wa elimu wanaweza kuzielewa kwa urahisi na kuwasaidia katika kuchukua hatua kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

Kwa kuwa shule zote zenye wanafunzi wa Darasa la II zitafanya upimaji, ripoti zitakazoandaliwa

zitaweza kuonesha uwezo wa wanafunzi katika kumudu stadi za KKK. Hata hivyo, ili kuandaa taarifa itakayosaidia mamlaka husika kuchukua hatua, ripoti itachambua utendaji wa wanafunzi katika kumudu stadi za KKK katika ngazi ya kitaifa na kimkoa. Taarifa zitachambua maeneo ambayo wanafunzi walimudu stadi za KKK na maeneo ambayo walishindwa kumudu stadi husika na sababu za kushindwa ili zifanyiwe kazi. Taarifa itaelezea namna vigezo mbalimbali vya upimaji vilivyofikiwa au kutokufikiwa na wanafunzi na sababu zilizowezesha kufikiwa au kutokufikiwa kwa vigezo hivyo.

Baraza litaandaa semina za kuwasilisha (dissemination seminars) ripoti zilizokamilika kwa kuhusisha watendaji wa mamlaka husika na wadau mbalimbali wa Elimu. Mamlaka hizo zitahusisha Maafisa Elimu wa Mkoa na Wilaya, Maafisa Elimu Taaluma wa Mkoa na Wilaya, Wathibiti Ubora, na Wakuu wa Shule kwa lengo la kuainisha changamoto zilizobanika wakati wa upimaji ili waweze kuchukua hatua za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK. Aidha, taarifa zitawekwa kwenye tovuti ya Baraza la Mitihani la Tanzania ambapo Katibu Tawala wa kila mkoa atajulishwa uwepo wa taarifa hizo ili aweze kuwataarifu wadau mbalimbali kwenye

mkoa wake kwa lengo la kuzitumia katika kuboresha stadi za KKK nchini.

## 4.0 HITIMISHO

Baraza la Mitihani linaamini kuwa upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika: Basic English Language Skills na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wa Darasa la Pili ni hatua muhimu katika kuboresha Elimu ya Msingi. Matokeo na taarifa za Upimaji huu yatatoa mwongozo kwa walimu, wanafunzi na wadau wa elimu kuhusu maeneo ya kufanyiwa maboresho ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata umahiri katika stadi za KKK. Matokeo yatakayotokana na tathmini hii yatasaidia kubaini viwango vya uelewa wa wanafunzi na changamoto wanazokutana nazo katika kujifunza KKK. Hii itawawezesha walimu kupanga mbinu bora za ufundishaji zinazozingatia mahitaji ya kila mwanafunzi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa ujifunzaji. Vilevile, wadau wa elimu kama vile wazazi, wasimamizi wa shule na serikali watapata taarifa sahihi zitakazowasaidia kufanya uamuzi wenye tija kuhusu uwekezaji katika elimu, mafunzo ya walimu na mikakati ya kuongeza ubora wa elimu.

Kupitia upimaji huu, shule zitaweza kutathmini mbinu zao za ufundishaji na kurekebisha changamoto zilizopo ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajengewa msingi bora wa elimu ambao utawasaidia katika ngazi za juu za masomo yao. Hivyo, upimaji huu licha ya kutoa dira kwa walimu na wanafunzi, pia utachangia kuboresha mfumo mzima wa elimu na kuimarisha maendeleo ya kitaaluma kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini.